**BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR**

Simu Nam. + 255 24 2230602/1
Fax Nam. + 255 24 2230215
Tovuti: www.zanzibarassembly.go.tz

SANDUKU LA BARUA 902,
ZANZIBAR
Barua Pepe: zahore@zanlink.com

# HOTUBA YA MAONI YA KAMATI YA USTAWI WA JAMII KUHUSU UTEKELEZAJI WA MAPENDEKEZO NA USHAURI WA KAMATI KWA MWAKA WA FEDHA 2022/2023 KWA WIZARA YA AFYA

**Mheshimiwa Spika,**

Nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu kwa kutujaalia uhai pamoja na afya njema, ambavyo vimetuwezesha kukutana tena katika Baraza hili Tukufu tayari kutekeleza majukumu yetu ya msingi kwa nchi yetu kiujumla. Ninamuomba Mwenyezi Mungu Mtukufu azidi kutukirimu neema zake ambazo kwa hakika sote ni wahitaji kwake.

**Mheshimiwa Spika,**

Napenda kuchukua fursa hii kumpongeza Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mhe. Dkt. Hussein Ali Mwinyi kwa kuimarisha Sekta ya Afya nchini kwa kuipatia majengo ya kisasa na vifaa tiba kwa ajili ya kutoa huduma zilizo bora zaidi kwa wananchi wetu.

**Mheshimiwa Spika,**

Napenda pia kukushukuru na kukupongeza wewe na Mhe. Naibu Spika pamoja na Wenyeviti wa Baraza kwa namna mnavyoliendesha Baraza kwa umahiri mkubwa, namuomba Mwenyezi Mungu awazidishie hekma na busara katika jukumu lenu la kutuongoza ili tuweze kutekeleza vyema wajibu wetu katika Chombo hiki muhimu kwa nchi yetu.

Vile vile, pongezi za pekee ziende kwa Mhe. Waziri na Naibu Waziri wa Afya kwa juhudi zao kubwa na mashirikiano wanayotuonesha katika utekelezaji wa kazi zetu, Kamati inawataka wazidi kutekeleza na kusimamia majukumu yao kwa ubora na ufanisi zaidi ili kufikia malengo yaliyokusudiwa.

**Mheshimiwa Spika**, Niwashukuru pia Wajumbe wa Kamati yetu ya Ustawi wa Jamii kwa namna wanavyonipatia mashirikiano makubwa katika kutekeleza majukumu ya Kamati yetu na naomba kuwatambua Wajumbe hao kama ifuatavyo:

| | |
|---|---|
| Mhe. Sabiha Filfil Thani | Mwenyekiti |
| Mhe. Nassor Salim Ali | Makamu Mwenyekiti |
| Mhe. Abdulla Hussein Kombo | Mjumbe |
| Mhe. Bihindi Hamad Khamis | Mjumbe |
| Mhe. Haji Omar Kheri | Mjumbe |
| Mhe. Panya Ali Abdalla | Mjumbe |
| Ndg. Salha Abdulla Abdulla | Katibu |
| Ndg. Talib Enzi Talib | Katibu |

**Mheshimiwa Spika,**

Baada ya utangulizi huo, sasa naomba kuwasilisha Maoni ya Kamati kuhusu Mapendekezo ya Kamati ya Ustawi wa Jamii kwa Wizara ya Afya kama ifuatavyo:

## DIVISHENI YA AFYA YA AKILI YA KIDONGO CHEKUNDU

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaipongeza Wizara kwa kufuatilia na kutekeleza maoni ya Kamati kuhusu suala la ukosefu wa watendaji wa kudumu wa Serikali katika Divisheni ya Afya ya Akili, katika Hospitali ya Kidongo Chekundu. Wizara imeweza kuzingatia suala hilo kwa kutoa ajira mpya kwa kada tofauti hospitalini hapo zikiwemo ajira za mkataba.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati pia inaipongeza Wizara kwa kuwapatia staki zao za posho la mazingira hatarishi watendaji wote wa divisheni ya Afya ya Akili pamoja na hospitali nyengine waliokuwa wameondolewa posho hizo.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati pia inaipongeza Serikali kwa kuona umuhimu wa kutenga zaidi ya shilingi Bilioni 49 kwa ajili ya uendeshaji wa hospitali zake mbali mbali ikiwemo hospitali ya Mnazi Mmoja, Hospitali ya Wazazi Mwembeladu na Hospitali ya Afya ya Akili Kidongo chekundu. Kamati inashauri Wizara kuhakikisha kuwa fedha hizo zinatumika kwa mujibu wa malengo yaliyokusudiwa ili kusaidia kuondokana na changamoto zinazoikabili sekta ya afya na kupunguza utegemezi kutoka kwa Washirika wa Maendeleo.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaunga mkono juhudi za Wizara katika kuwaendeleza wafanyakazi kimasomo na imefurahishwa kuona kuwa

Serikali inawatumia hata watanzania walio nje ya nchi wanaofanyakazi katika sekta afya katika kusaidia kuongeza uwezo wa wafanyakazi wetu wa Sekta ya Afya hapa Zanzibar.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imeridhishwa na hatua ya Wizara kupitia Kitengo cha afya kazini kuweza kuwapatia Vitambulisho vya kazi wafanyakazi ili kuwarahisishia kazi wanapokwenda katika maeneo ya ukaguzi. Sambamba na kupanga bajeti ya ujenzi wa ofisi kwa mwaka wa fedha 2024/25, pamoja na kulitafutia ufumbuzi suala la usafiri katika vitengo vyote vya wizara.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaipongeza Wizara kwa kuhakikisha kuwa inaimarisha mashirikiano kati yake na wadau mbali mbali wa Afya ya usalama kazini wakiwemo Mfuko wa Hifadhi ya Jamii (*ZSSF)*, Wizara ya Maendeleo ya Jinsia,Wazee na Watoto, Afisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji , Wizara ya Nchi Afisi ya Rais Katiba Sheria Utumishi na Utawala Bora ,Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale pamoja na Shirika la Msalaba Mwekundu katika upande wa utoaji huduma ya kwanza pale wafanyakzi wanapopata ajali wakiwa kazini.

## BOHARI KUU YA DAWA

**Mheshimiwa Spika**, Kamati imeridhika na Wizara kwa kuanzisha utaratibu maalum wa dawa zinazonunuliwa kwa ajili ya Hospitali na vituo vya Afya viliopo Pemba kupelekwa moja kwa moja katika Bohari Kuu Vitongoji, badala ya kupita Bohari Kuu Maruhubi, kama awali ilivyokuwa ikifanyika kwani ilipelekea kuchelewa kupatikana dawa hizo katika Hospitali na vituo vya Afya. Sambamba na kuondokana na matatizo ya mtandao katika usambaji wa dawa baada ya kufanyakazi kwa karibu na Wakala wa Miundombinu ya TEHAMA (ZICTIA).

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaishauri wizara kuhakikisha kuwa dawa hizo zinafika na zinatumika kwa ajili ya wananchi. Aidha ihakikishe suala la ulinzi linakuwa endelevu na linaimarishwa katika Bohari Kuu za dawa na taasisi zenye dhamana na suala la ulinzi zihakikishe kuwa shughuli za ulinzi zinafanyika ipasavyo ili kuondokana na changamoto ya upotevu wa dawa katika hospitali na vituo vya afya.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaipongeza Wizara ya Afya kwa kuhakikisha kwamba misaada yote inayoletwa kutoka kwa Wahisani mbali mbali kwenda Bohari Kuu ya Dawa inafuata utaratibu na miongozo iliyopo chini ya Ofisi ya Mfamasia Mkuu wa Serikali. Hatua hii inaepusha uingizwaji wa dawa zilizokuwa zimeshamaliza muda wa matumizi ambazo ni hatari kwa maisha ya binadamu.

Aidha, Kamati imeridhika kuona kuwa Serikali imeridhia kwa mwaka wa fedha 2023/2024 kuiongezea bajeti Bohari ya Kuu ya Dawa zaidi ya shilingi milioni 350 kwa lengo la kuweza kufanya kazi zao kwa ufanisi ili kuondokana na uchelewaji wa uingizwaji wa dawa nchini.

**Mheshimiwa Spika**,
Kamati inaipongeza Wizara kwa kuimarasha utaoaji wa huduma za Afya kwa kuweka miundombinu bora ya TEHAMA kwa kuziunganisha Hospital zote za Wilaya na mkonga wa Taifa. Hatua hii itasaidia kurahisisha utumaji wa taarifa muhimu za afya pamoja na maombi ya dawa.

## TAASISI YA UTAFITI WA AFYA ZANZIBAR

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati inaishauri Serikali kupitia Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo kuharakisha kuipatia eneo maalum Taasisi hii ili iweze kuanzisha Shamba Darasa la mimea ya tiba asili.

Kamati imebaini kuwa Taasisi ya Utafiti wa Afya kwa muda mrefu imefanya maombi ya kupatiwa eneo kwa ajili ya kuendeleza shughuli hizo za utafiti lakini hadi sasa hivi bado haijapatiwa eneo hilo. Hivyo Kamati inaishauri Serikali kulifanyia kazi ombi hilo ili taasisi hii iweze kupatiwa eneo hilo.

## PROGRAMU KUU YA UENDESHAJI NA URATIBU

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati inaipongeza Wizara kwa kukamilisha Miradi ya Ujenzi ya Hospitali za Wilaya na Mkoa pamoja na kufanya ukarabati vituo mbali mbali vya daraja la kwanza katika Hospitali hizo na kuanza kutoa huduma.

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati imesisitiza mashirikiano baina ya Wizara ya Afya na Tume ya

Mipango ili kuendeleza mipango ya muda mrefu ya wizara kwa kuhamasisha vijana kujifunza fani maalum za afya ili kuwa na wataalamu wanaohitajika katika fani hizo.

**Mheshimiwa Spika**,
Kamati imeridhika na mipango ya Serikali kwa mradi wa ujenzi wa nyumba za watumishi katika hospitali za umma Unguja na Pemba. Kamati inaishauri Wizara kuendelea kuwapatia watumishi wa afya makaazi ya karibu na vituo vya kufanyia kazi ili kuondosha usumbufu unaojitokeza kwa wananchi wakati wanapotaka huduma.

## HITIMISHO

**Mheshimiwa Spika,** napenda kuchukua nafasi hii kuwashukuru Waheshimiwa Wajumbe kwa kunisikiliza kwa makini wakati wote nilipokuwa nawasilisha hotuba hii. Sasa niwaombe Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu waijadili na waichangie hotuba hii kwa mustakabali wa nchi yetu na taifa kwa ujumla.

……………………………………

**Mhe. Sabiha Filfil Thani**

**Mwenyekiti,**

**Kamati ya Ustawi wa Jamii,**

**Baraza la Wawakilishi,**

**Zanzibar.**